HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA

S. L. P. 76 Mafinga, Simu 026-2772393, Fax 026-2772070

# TAARIFA YA FEDHA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA 2017

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Naomba kuwasilisha taarifa ya Mapato na matumizi kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2017 Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni :-

A. Taarifa ya Mapato

B. Taarifa ya Matumizi

C. Taarifa ya Bakaa ya Fedha za miradi ya maendeleo 2016/2017

## A: TAARIFA YA MAPATO :

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Halmashauri ya Mji wa Mafinga kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilikisia kukusanya kutoka vyanzo vyake mbalimbali jumla ya Tshs. 22,063,313,089/=.

Makisio ya mapato ya vyanzo vya ndani jumla ya Tshs. 3,120,869,000/= Hali halisi ya makusanyo ya vyanzo vya ndani kwa kipindi cha mwezi wa Oktoba 2017 ni Tshs . 168,583,363.90 ambayo sawa na asilimia 22.33 kwa makusanyo ya mwaka. Pia tulianza na salio anzio mwezi Julai 2017 Tshs. 84,909,015.71 kwenye akaunti ya vyanzo vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kupokea fedha za ruzuku ya matumizi mengineyo (OC) jumla ya Tshs. 1,016,165,000/= Hali halisi ya mapokezi ya (OC) kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2017 tumepokea Tshs. 180,588,000/=

fedha za Ruzuku ya matumizi mengineyo(OC) ambayo ni sawa na asilimia 24.22 kwa makisio ya mwaka. Aidha tulianza na salio anzio kwenye fedha za Matumizi mengineyo (OC) Tshs. 1,481,554.75 kwa mwezi Julai 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kupokea fedha za miradi ya maendeleo kutoka Serikali kuu na wafadhili jumla ya Tshs. 4,096,407,800/=. Hali halisi ya mapokezi ya Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2017 tumepokea Tshs. 88,561,675.62/= Jumla ya fedha za miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 17.70 mapokezi ya mwaka. Fedha tulizochangia za Miradi ya maendeleo ya vyanzo vya ndani kwa mwezi wa Oktoba 2017 Tshs. 0/= ambayo ni sawa na asilimia 6.88 ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kupokea fedha za mishahara kutoka Serikali kuu jumla ya Tshs. 13,088,695,000/= .

Aidha, Fedha tulizopokea za mishahara kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2017 ni Tshs. 836,430,000/= ambayo ni sawa na asilimia 24.89 mapokezi ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kupokea fedha za makusanyo mengineyo yatokanayo na TIKA, Bima ya afya na PAPO KWA PAPO jumla ya Tshs. 489,961,620/= Fedha ambazo tumekusanya kwa mwezi huu Oktoba 2017 ni 36,415,370/= ambayo ni sawa na asilimia 22.55 ya mwaka.

Tazama viambatishi vinavyoonesha Mapato. Kiambatishi "A" Mapato ya vyanzo vya ndani vya Halmashauri Uk 5 na 6 . Kiambatishi "B" cha mapato ya Ruzuku ya Matumizi mengineyo (OC) Uk. 8, Kiambatishi "C" Mapato ya miradi ya maendeleo Uk. 9 na Kiambatishi "D" Mishahara Uk. 10 na Kiambatishi "E" Mapato Mengineyo Uk. 11.

B: TAARIFA YA MATUMIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti

Halmashauri ya Mji wa Mafinga kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilikisia kutumia kutoka vyanzo vyake mbalimbali jumla ya Tshs. 22,063,313,089/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kutumia fedha kutokana na mapato yetu ya vyanzo vya ndani jumla ya Tshs. 3,120,869,000/=. Matumizi halisi kwa kipindi cha mwezi Oktoba 2017 Tshs. 230,172,421.94 ambayo sawa na asilimia 18.02 ya matumizi ya mwaka. Kwa mchanganuo wa Matumizi ya kawaida ya mapato ya ndani Tshs 230,172,421.94 na Mchango wa Halmashauri katika miradi ya maendeleo Tshs 0/=

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kutumia fedha za ruzuku ya matumizi mengineyo (OC) jumla ya Tshs. 1,016,165,000/= Kwa kipindi cha Oktoba 2017 Tshs. 96,140,000 fedha za Ruzuku ya matumizi mengineyo (OC) iliyotumika ambayo sawa na asilimia 15.36 ya matumizi ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kutumia fedha za miradi ya maendeleo kutoka Serikali kuu na wahisani jumla ya Tshs. 4,096,407,800/=. Fedha zilizotumika kwa miradi ya Maendeleo kwa mwezi Oktoba 2017 Tshs. 560,275,186 ambayo sawa na asilimia 15.56 ya matumizi ya mwaka.

Pia kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kutumia fedha za miradi ya maendeleo kutoka vyanzo vya ndani jumla ya Tshs. 1,872,541,400/= Fedha zilizotumika kwa miradi ya Maendeleo ya vyanzo vya ndani kwa mwezi Oktoba 2017 Tshs. 1,970,000/= ambayo sawa na asilimia 4.67 ya matumizi ya mwaka

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kutumia fedha kulipia mishahara kutoka Serikali kuu jumla ya Tshs. 13,088,694,800/= Aidha, matumizi ya Mishahara kwa mwezi wa Oktoba 2017 ni Tshs. 836,430,000/= ambayo sawa na asilimia 24.89 ya matumizi ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikisia kutumia fedha za makusanyo mengineyo yatokanayo na TIKA, Bima ya afya na PAPO KWA PAPO jumla ya Tshs 489,961,620/= Fedha ambazo tumetumia kwa mwezi huu Oktoba 2017 ni Tshs. 11,586,000/= ambayo ni sawa na asilimia 26.14 ya mwaka.

Kama viambatishi vya matumizi vinavyoonesha. Kiambatishi "F" matumizi ya makusanyo ya ndani Uk 12 – 17 , Kimbatanishi "G" Matumizi Mengineyo (OC) Uk. 18 , Kiambatishi "H" Miradi ya Maendeleo Uk.19, Kiambatishi "I" Uk. 20 na Kiambatishi "J" Matumizi mengineyo Uk. 21

## C: TAARIFA YA FEDHA ZA BAKAA ZA MIRADI YA MAENDELEO 2016/2017:

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Fedha za miradi ya maendeleo ambazo tumevuka nazo na zinaendelea kuletwa kutoka mwaka wa fedha 2016/2017 . Kwa mchanganuo ufuatao fedha za miradi ya vyanzo vya ndani Tshs. 27,000,000/= na miradi ya maendeleo ya kutoka serikali kuu na wahisani Tshs. 1,251,176,978.04

Aidha mpaka kufikia mwezi Oktoba 2017 tumeweza kutumia salio la fedha za mwaka 2016/2017 Kwa mchanganuo ufuatao Tshs 630,697,667.28 kutoka serikali kuu na wahisani na Tshs. 27,000,000/= za miradi ya maendeleo ya vyanzo vya ndani vya Halmashauri.

Salio lililobaki la fedha za miradi mpaka kufikia mwezi Oktoba 2017 ni kama ifuatavyo:- fedha za miradi ya vyanzo vya ndani Tshs. 0/= na miradi ya maendeleo ya kutoka serikali kuu na wahisani Tshs. 620,479,310.76

Kama kiambatishi cha bakaa ya fedha za miradi ya maendeleo na matumizi kufikia mwezi Julai 2017 kinavyoonesha. Kiambatishi "K" Uk .22

Naomba kuwasilisha.

Robert Sinnah

Kaimu Mweka Hazina

Halmashauri ya Mji wa Mafinga